Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

TANGAZO LA UCHAGUZI WA NAFASI MBALIMBALI ZA UONGOZI WA TAASISI YA SETTA

Uongozi wa Taasisi ya SETTA unawatangazia Alumni wote kuwa mchakato rasmi wa kufanyika Uchaguzi Mkuu wa Taasisi umeamza. Uchaguzi Mkuu wa kupata viongozi wapya wa Taasisi utafanyika **Mwezi huu 28 Novemba, 2026.**

Uchaguzi huu ni sehemu ya utekelezaji wa Katiba ya Taasisi juu ya Muhula wa Uongozi unaodumu kwa muda wa Miaka Mitano (5), aidha Uchaguzi huu unalenga kupata viongozi wenye Maono, Uadilifu, na Uwezo wa kuivusha taasisi kuelekea mafanikio zaidi.

Kutokana na hatua hiyo, Kamati ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa Alumni wote wenye Sifa, Uwezo na Dhamira ya dhati ya kuitumikia Taasisi katika kukua na kuleta maendeleo endelevu kwa Alumni na Jamii ya Watanzania kwa ujumla kupitia ushirikiano wa kimkakati baina ya Tanzania na Uturuki.

NAFASI ZINAZOWANIWA NA SIFA ZA WAOMBAJI

1. **Mwenyekiti wa Taasisi (Nafasi 1).**

Majukumu Makuu:

- Kuwa Kiongozi Mkuu na Msemaji Mkuu wa Taasisi.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera, Dira na Mikakati ya Taasisi.
- Kuongoza Mikutano Mikuu na Mikutano ya Bodi ya Taasisi.

Sifa na Vigezo vya Muombaji:

- Awe ni muhitimu wa Chuo Kikuu / Mafunzo ya Lugha / Elimu ya Dini kutoka nchini Uturuki.
- Uzoefu wa usimamizi au uongozi usiopungua miaka mitano (5) katika taasisi, shirika la kijamii au sekta binafsi/serikali.
- Awe mwanachama hai wa SETTA aliyetimiza wajibu na michango yake yote kwa wakati.
- Awe na uwezo mkubwa wa ushawishi, usimamizi wa rasilimali, na ujuzi wa kujenga ushirikiano wa kimkakati.
- Awe na uadilifu na asiyewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai au la mmomonyoko wa maadili.

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

2. Katibu wa Taasisi (Nafasi 1).

Majukumu Makuu:

- Kusimamia shughuli zote za utendaji wa kila siku na uratibu wa kiutawala ndani ya Taasisi.
- Kutunza kumbukumbu, nyaraka na mihutasari yote ya mikutano ya Taasisi na Bodi.
- Kuratibu mawasiliano yote ya ndani na nje ya Taasisi.

Sifa na Vigezo vya Muombaji:

- Awe ni muhitimu wa Chuo Kikuu / Mafunzo ya Lugha / Elimu ya Dini kutoka nchini Uturuki.
- Uzoefu wa angalau miaka mitatu (3) katika usimamizi wa utawala au ukatibu wa taasisi.
- Awe na uwezo mkubwa wa kuandika na kuzungumza kwa fasaha lugha za Kituruki na Kiingereza.
- Awe mwanachama hai wa Taasisi ya SETTA mwenye nidhamu na uwajibikaji wa hali ya juu.

3. Mweka Hazina wa Taasisi (Nafasi 1).

Majukumu Makuu:

- Kusimamia mfumo wote wa fedha, bajeti na rasilimali za Taasisi.
- Kutayarisha ripoti za fedha za kila robo mwaka na za mwaka kwa ajili ya Bodi na Mkutano Mkuu.
- Kusimamia ukaguzi wa hesabu za fedha (Audit) na utekelezaji wa sera za kifedha.

Sifa na Vigezo vya Muombaji:

- Awe ni muhitimu wa Chuo Kikuu / Mafunzo ya Lugha / Elimu ya Dini kutoka nchini Uturuki.
- Uzoefu wa angalau miaka mitatu (3) katika usimamizi wa fedha, uandaaji wa bajeti na ripoti za kifedha.
- Awe mwaminifu, mwadilifu na mwenye rekodi safi ya usimamizi wa rasilimali.
- Awe mwanachama hai wa Taasisi ya SETTA.

SETTA
SOCIAL-ECONOMIC TIER OF TURKISH ALUMNI

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

1. Kuwa raia wa Tanzania na mhitimu kutoka chuo kikuu au taasisi ya elimu ya juu nchini Uturuki.
2. Kuwa mwanachama aliyesajiliwa na aliye hai ndani ya taasisi ya SETTA.
3. Kuwa mwadilifu, mwenye nidhamu ya kazi, na asiye na kashfa yoyote ya kiutendaji au ya kisheria.
4. Kuwa na uwezo wa kuwasiliana vyema kwa lugha ya Kituruki na Kiingereza.
5. Kuwa tayari kujitolea muda na rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya Taasisi na wanachama wake.
6. Asiwe na mgongano wa kimaslahi (Conflict of Interest) unaoweza kuathiri utendaji wake ndani ya Taasisi.

TARATIBU NA NYARAKA ZA UTUMAJI MAOMBI

Muombaji anapaswa kuwasilisha nyaraka zifuatazo kwa Kamati ya Uchaguzi:

1. **Barua ya Maombi** ikibainisha nafasi unayoomba na sababu za kugombea.
2. **Kielelezo cha Wasifu (CV)** kilichoboreshwa kinachoonyesha elimu na uzoefu.
3. **Nakala ya Vyeti vya Elimu** (Vyeti vya Elimu ya Chuo / Mafunzo ya Lugha / Elimu ya Dini).
4. **Picha 2 za Rangi** (Passport size).
5. **Ilani ya Sera/Dhamira ya Uongozi** ya kurasa 2 kueleza mipango yako kwa SETTA ukiuchaguliwa.

RATIBA NA JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Hatua	Tarehe ya Utekelezaji
Ufunguzi wa Maombi	05 Novemba, 2026
Tarehe ya Mwisho ya Kupokea Maombi	14 Novemba, 2026 (Saa 5:59 Usiku)
Mchujo na Uhakiki wa Fomu	15 – 17 Novemba, 2026
Uchapishaji wa Orodha ya Wagombea Waliopitishwa	18 Novemba, 2026
Kipindi cha Kampeni	19 – 27 Novemba, 2026
Siku ya Uchaguzi Mkuu	**28 Novemba, 2026**

Mikocheni B,
Coca-Cola Road,
House No.48,
P.O. Box 6166,
Dar es Salaam, Tanzania..

NJIA YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa njia ya barua pepe kwenda:

- **Barua Pepe:** info@settafoundation.or.tz
- **Kichwa cha Barua Pepe:** Maombi ya Uongozi - [Weka Nafasi Unayoomba]

ZINGATIA: *"Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda wa mwisho hayatapokelewa. Maombi yenye taarifa za kughushi yatasababisha muombaji kuondolewa sifa mara moja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu".*

Imetolewa na:

Mwenyekiti,
Kamati ya Uchaguzi,
Taasisi ya SETTA.
Tarehe: 05 Novemba, 2026.